



East African Journal of Swahili Studies

eajss.eanso.org

Volume 6, Issue 2, 2023

Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475

Title DOI: <https://doi.org/10.37284/2707-3475>



EAST AFRICAN
NATURE &
SCIENCE
ORGANIZATION

Original Article

Ukiukaji wa Kanuni Bia za Greenberg katika Miundo ya Tungo Zenye Vihusishi Katika Lugha ya Kiswahili

Jemimah Kwamboka Ongwae^{1*} na Prof. Peter Githinji, PhD¹

¹ Chuo Kikuu cha Kenyatta, S. L. P. 43844-00100 Nairobi, Kenya.

* ORCID ID <https://orcid.org/0009-0007-8903-1581>; Barua pepe ya mawasiliano: jemimahkongwae@gmail.com

DOI ya Nakala: <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1596>

Tarehe ya Uchapishaji: IKISIRI

25 Novemba 2023

Istilahi Muhimu:

*Kanuni bia,
Muundo,
Vihusishi,
Ukiukaji,
Taipolojia.*

Makala haya yalidhamiria kubaini ukiukaji wa baadhi ya kanuni bia za Greenberg katika miundo ya tungo zenye vihusishi vya Kiswahili. Katika utafiti wake, Greenberg (1963), alipendekeza kanuni bia 45 na kutafiti lugha 30 ili kuchunguza mpangilio wa vipashio vya kiisimu katika makundi mbalimbali ya lugha. Lugha ya Kiswahili ilikuwepo mojawapo ya sampuli alizoteua. Hata hivyo, katika kuzingatia uwekaji vihusishi, inaonekana kukiuka baadhi ya kanuni hizo. Kwa hivyo, mkabala wa Greenberg (1963) ulitumika. Kanuni bia za Greenberg hasa zile zinazozungumzia vihusishi pekee zilitumika kuchanganua miundo na mazingira ya kiisimu yanayosababisha ukiukaji wa baadhi ya kanuni za Greenberg katika uwekaji wa vihusishi vya Kiswahili. Data iliyotumika ilikuwa ni tungo zenye vihusishi. Mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi ilitumika kuteua vihusishi hivi na vilikusanywa kwa kusoma vitabu vya sarufi na makala kutoka kwenye majarida na makala ya mtandaoni. Data ilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia mkabala wa kanuni bia za Greenberg kupitia ufafanuzi wa data kwa njia ya maelezo na unukuzi wa kanuni bia za Greenberg. Ilijidhihirisha kuwa baadhi ya kanuni bia za Greenberg zina ukiushi katika lugha ya Kiswahili. Ukiushi hasa ulitokea kwa sababu sifa A haikumiliki sifa B kwa kuzingatia sheria ya uchanganuzi iliyooleanwa. Haya yalibainika hasa kwa kuwa lugha ya Kiswahili inamiliki aina mbili za vihusishi; vihusishi vya kabla ya nomino na vihusishi vya baada ya nomino katika umbo lake la nje. Hata hivyo, baadhi ya kanuni bia zingine zilionyesha utiifu. Aidha baadhi ya kanuni hizi zina utata ambao unaleta changamoto katika juhudi za kutoa kauli jumlishi. Makala haya yatachangia katika kongoo ya utaratibu wa vipashio katika sentensi, taipolojia ya lugha na sintaksia ya Kiswahili.

APA CITATION

Ongwae, J. K. & Githinji, P. (2023). Ukiukaji wa Kanuni Bia za Greenberg katika Miundo ya Tungo Zenye Vihusishi Katika Lugha ya Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), 30-43. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1596>.

CHICAGO CITATION

Ongwae, Jemimah Kwamboka and Peter Githinji. 2023. "Ukiukaji wa Kanuni Bia za Greenberg katika Miundo ya Tungo Zenye Vihusishi Katika Lugha ya Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (2), 30-43. <https://doi.org/10.37284/jammk.6.2.1596>.

HARVARD CITATION

Ongwae, J. K. & Githinji, P. (2023) "Ukiukaji wa Kanuni Bia za Greenberg katika Miundo ya Tungo Zenye Vihusishi Katika Lugha ya Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(2), pp. 30-43. doi: 10.37284/jammk.6.2.1596.

IEEE CITATION

J. K. Ongwae, & P. Githinji "Ukiukaji wa Kanuni Bia za Greenberg katika Miundo ya Tungo Zenye Vihusishi Katika Lugha ya Kiswahili", *EAJSS*, vol. 6, no. 2, pp. 30-43, Nov. 2023.

MLA CITATION

Ongwae, Jemimah Kwamboka & Peter Githinji. "Ukiukaji wa Kanuni Bia za Greenberg katika Miundo ya Tungo Zenye Vihusishi Katika Lugha ya Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 2, Nov. 2023, pp. 30-43, doi:10.37284/jammk.6.2.1596.

UTANGULIZI

Vihusishi ni mada ambayo imewavutia wanasarufi na wanaisimu mbalimbali, na hivyo imeweza kutafitiwa kwa viwango mbalimbali vya kiisimu. Vihusishi vimeonekana kuwa na dhima kadha katika sarufi ya lugha katika kueleza nyakati, mahali, sababu/ kusudi ya jambo au kitu fulani, umilikishi, ulinganishi, ala, namna n.k. Vihusishi ni maneno au fungu la maneno ambayo huonyesha uhusiano uliopo baina ya kitu kimoja na kingine au mtu na mwingine. O'Dowd (1998) anaeleza vihusishi kama viunganishi vinavyotumika kwa maneno katika lugha ili kuonyesha uhusiano uliopo kati ya nomino, kiwakilishi na elementi zingine katika sentensi. Vihusishi kwa kawaida hutumika pamoja na nomino ili kuleta dhima yake na maana inayotarajiwa.

Vihusishi vya lugha mbalimbali huwa na miundo tofauti. Tunapozungumzia miundo ya lugha tunapata kuwa, miundo ya lugha huangaziwa katika eneo pana la taipolojia ya lugha. Abraham na wenzake (1995) wanaeleza kuwa taipolojia ya lugha ni njia mojawapo iliyozunguza ya kuchunguza athari za lugha na uhusiano uliopo katika lugha hizo. Greenberg ni mmojawapo wa wanaisimu ambao wameshughulikia taaluma hii na kazi yake imeathiri tafiti nyingi katika uwanja huu. Alipendekeza kanuni za kijumla ili kueleza mpangilio wa vihusishi katika lugha 30 na aliibuka na kanuni bia za kisarufi 45 zinazotumika kueleza vipengele vinavyofanana na miundo inayojitokeza kwa lugha zote. Alieleza kanuni hizi katika vigezo vitatu, mpangilio wa maneno msingi, sintaksia na mofolojia. Utafiti huu ulizingatia kanuni zinazohusu vihusishi pekee.

Luraghi (2003) anaeleza kategoria hizi za vihusishi kwa kufafanua kuwa kuna vihusishi vinavyokuja kabla ya nomino na kuna vihusishi vinavyokuja baada ya nomino. Anaendelea kusema kuwa sehemu ya uwekaji wa vihusishi hivi haiwi ya kawaida kwa maana wakati mwingi inaathiriwa na mazingira ya kiisimu na basi vihusishi vingi huashiria maana tofauti kutegemea sehemu ambayo vimechukua katika sentensi. Kutokana na kauli ya Greenberg kuwa kanuni hizi zapaswa kuwa halali na zinaweza kuwakilisha lugha nyingi ulimwenguni, ni wazi kuwa huenda kukawa kuna baadhi ya lugha ambazo hukiuka kanuni hii kutokana na upekee wa miundo yazo. Kanuni ya (3) kwa mfano inasema kuwa lugha zenye mpangilio wa kitenzi-kiima-yambwa huwa na vihusishi vya kabla ya nomino, lakini lugha ya Kiswahili ambayo inatosheleza kanuni hii pia ina vihusishi vinavyopatikana baada ya nomino.

Kutokana na kuwa kuna tofauti za makundi ya lugha ambayo hudhihirisha miundo tofauti katika michakato ya kimfosintaksia kama vile lugha tetanishi, ambishi bainishi, ambishi mchanganyo, muundo gubi na pia zile zenye kiunzi cha mzizi na ruwaza (taz. Katamba na Stonham, 2006). Inamaanisha kuwa kuna tofauti ya jinsi lugha hupanga vipashio vyake. Ingawa lugha zinaweza kushirikisha kanuni fulani za kisarufi, kila lugha hupanga vipashio vyake kivyake; jambo ambalo hudhihirika kwenye ruwaza za kimuundo, hasa katika mpangilio wa maneno katika sentensi na virai. Hivyo basi, kuna haja ya kuelewa muundo mzima wa vipashio vya lugha mbalimbali ili kubainisha upangaji wake katika taipolojia ya lugha. Kwa mantiki hii, kanuni za Greenberg ni msingi mzuri wa kuchanganua na kuhakiki utaratibu wa upangaji

wa vipashio vyenye vihusishi katika tungo za Kiswahili.

Sababu zilizotupelekea kuchagua mada hii katika utafiti wetu ni kutokana na kuwa hatukupata tafiti ambazo zimefanywa kwa kutumia kanuni bia za Greenberg ili kuchanganua muundo wa vihusishi vya Kiswahili. Mada ya vihusishi ni muhimu kwa sababu vihusishi huchangia kujenga msingi mkuu wa lugha ambao ni sintaksia. Vilevile, tulitambua kwamba katika lugha ya Kiswahili, vihusishi vinaweza kujitokeza katika mazingira tofauti ya kiisimu na wajibu unaotekelezwa na vihusishi unaweza kutekelezwa kwa njia mbalimbali ambazo huathiri miundo ya sentensi.

Kwanza kabisa, kuna vihusishi vinavyojitokeza kabla ya nomino. Katika kirai chini ya mchanga kwa mfano, kihusishi “chini ya” kinatangulia nomino “mchanga”. Kwa upande mwingine, kuna vihusishi vinavyokuja baada ya nomino katika tungo, hasa tunapozingatia virai nomino ambapo uhusiano kati ya nomino mbili huonyeshwa kwa kutumia a-unganifu. Mfano mzuri ni kirai nomino mwezi wa kwanza ambapo nomino ‘mwezi’ imetangulia kihusishi cha a-unganifu ‘wa’. Tukitazama jinsi kuwepo au kutokuwepo kwa vihusishi kunathiri miundo ya sentensi, tunapata kuwa mofu i, e, li na le katika kauli ya kutendea huonyesha ushikaji wa vihusishi katika shina la kitenzi. Vilevile, uambishaji wa –ni kama kiambishi tamati kwenye nomino za mahali kama vile kwenye maneno nchini na sebuleni huashiria ushirikishi wa vihusishi kwenye nomino.

Zaidi ya hayo, kuna maumbo mbalimbali ya vihusishi vya Kiswahili. Kwa mfano, kuna vile vya neno moja kama vile na, kwa, ya, na kadhalika. Vilevile, kuna vihusishi vingine ambavyo huwa mwambatano wa maneno kama vile mbele ya, kando ya, karibu na, kwa niaba ya, kwa ajili ya, na kadhalika. Mbali na umbo la vihusishi, kuna mwingiliano wa kategoria za maneno ambapo baadhi ya vihusishi pia huanishwa katika kategoria zingine na maneno. Kwa mfano vihusishi vya a-unganifu, vinaweza kutumika pia kama viunganishi, viwakilishi na vivumishi. Pia, vipashio fulani vya vihusishi hutumika kama viangami vinapoambishwa

kwenye vimilikishi vya Kiswahili kama vile kwenye maneno kwangu, naye, yake n.k. Hata hivyo mwingiliano huu wakati mwingine huathiri ufasiri wa vihusishi kama vinavyochambuliwa kitaipolojia.

Vilevile, kazi ya vihusishi katika Kiswahili inaweza kutekelezwa katika kauli ya kutendea katika mnyambuliko wa vitenzi. Kwa mfano, 1) Ann alituma pesa kwa mama. 2) Ann alitumia mama pesa. Sentensi hizi mbili zina maana sawa, lakini zina miundo tofauti. Kazi ya kisarufi inayotekelezwa na kihusishi kwa katika sentensi ya kwanza yenye kihusishi inatekelezwa na mofu inayoashiria kauli ya kutendea katika sentensi ya pili. Hivyo basi, uchangamano wa fasiri ya dhana ya vihusishi katika lugha ya Kiswahili una athari fulani katika muundo wa vipashio vinavyohusiana na vihusishi, jambo ambalo litasababisha changamoto katika utendakazi wa kanuni bia zilizopendekezwa na Greenberg. Hivyo basi ni suala muhimu kiutafiti kuchunguza uzingatiaji wa kanuni bia za Greenberg ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni mojawapo ya lugha alizotumia katika kuzianisha lugha kitaipolojia kugemea kanuni bia alizobainisha.

Matokeo ya utafiti huu yataongeza manufaa kwa tafiti zingine za awali na kwa watafiti wa mbeleni pia. Mada hii ni muhimu kwa sababu utafiti huu utawanufaisha watafiti wengine na wanaisimu kwa jumla. Pia uwazi wa muundo wa vihusishi utabainika na hivyo kuleta uelewa zaidi wa vihusishi vya Kiswahili.

Mbinu za utafiti

Muundo wa kimaielezo ulitumika katika makala haya. Utafiti huu ulifanyika maktabani. Data za makala haya zilikusanywa kutoka kwa vitabu, makala, majarida na matini zingine zinazozungumzia dhana ya vihusishi. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kwa kuwa mtafiti anajua data yake ina sifa zipi na pia analenga kipengee mahsusi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Creswell (2002), sampuli ya kimaksudi ni aina ya sampuli inayoteuliwa na mtafiti kwa misingi inayoaminika kuwa mwafaka katika kuafiki malengo ya utafiti. Vihusishi vya kimsingi

viliteuliwa kutoka kwa kitabu cha Huddleston, na Pullum, (2002) *'The Cambridge grammar of the English language'* Mbinu ya kusoma na kuandika ilitumika katika harakati ya kutafuta na kukusanya data. Mtafiti alinakili ile data muhimu inayochukua sifa zinazotarajiwa kuchangia na kunufaisha utafiti. Katika kuchanganua data, kanuni bia za Greenberg zilitumika, mtafiti alizingatia zile zinazolenga vihusishi pekee moja kwa moja. Katika kuwasilisha matokeo, miundo na mazingira ya kiisimu yanayosababisha ukiukaji wa baadhi ya kanuni za Greenberg katika miundo ya vihusishi vya Kiswahili ilichanganuliwa.

Tatizo

Miundo ya lugha ni swala lenye uzito mkubwa kiisimu. Kutokana na kuwa vihusishi ni mojawapo ya kategoria za maneno yenye athari kubwa katika miundo ya lugha, lugha nyingi ulimwenguni zimetafitiwa kwa kutumia mikabala mbalimbali ili kubaini miundo ya vihusishi na watafiti kadhaa kama vile Koopman (2000), Lefebvre na Brousscau (2001) na wengineo. Riemsdijk (2020) anaeleza kuwa uchanganuzi wa miundo hii ni muhimu na inafaa uelezwe kwa njia inayoeleweka zaidi kwa vigezo muhimu vya muundo msingi usiobadilika ambao huenda ukawa ni msingi wa kisintaksia wa lugha zote za binadamu. Kiswahili kilikuwa miongoni mwa lugha 30 alizoteua Greenberg (1963) katika sampuli ya utafiti wake ulioibuka na kanuni bia zinazotumika katika kuainisha lugha kitaipolojia. Hata hivyo, lugha hii imeghairi baadhi ya kanuni bia alizopendekeza hivi kwamba hazielezi muundo wa vihusishi vyake kikamilifu. Mfano mzuri ni kanuni ya pili ambayo inaeleza kuwa, katika lugha zilizo na vihusishi vinavyotangulia nomino aghalabu huwa na vimilikishi vinavyofuata nomino inavyovitawala ilhali katika lugha zenye vihusishi vinavyotokea baada ya nomino aghalabu vimilikishi vyake hutangulia nomino. Katika sentensi *mtoto wangu aliketi juu ya meza*; kwa mfano, kimilikishi kimekuja baada ya nomino. Kimantiki, wangu mtoto haikubaliki katika lugha hii. Kwa vile Kiswahili kina

vihusishi vya baada ya nomino, ni vigumu kueleza ni mantiki ipi inayotumika.

Ijapokuwa kuna sifa mbalimbali ambazo lugha za binadamu hushirikiana, kila lugha huwa na upekee wake kuhusu mpangilio wa vipashio vyake, jambo ambalo linafanya kutoa madai ya jumla kuhusu ubia wa kimuundo kupotoka katika baadhi ya lugha. Utafiti huu utalenga uchanganuzi wa muundo wa vihusishi vya Kiswahili hasa ukitumia kanuni alizopendekeza Greenberg ili kubainisha ukiukaji uliopo na kuleta uelewa wa nafasi ya vihusishi katika muundo wa sentensi na vipashio vyenye vihusishi katika tungo za Kiswahili. Tafiti za awali zinaibainisha kuwa sehemu hii haijafanyiwa utafiti wa kina kwa lugha ya Kiswahili na wala mkabala wa Greenberg haujatumiwa katika kuhakiki kanuni bia alizotaja katika uchunguzi wake. Kwa hivyo, utafiti huu unanua kuongeza maarifa na kufidia pengo lililopo kwa kuchanganua vihusishi vya Kiswahili.

MISINGI YA NADHARIA

Mkabala wa Kanuni Bia za Kisarufi za Greenberg

Joseph Harold Greenberg (1963) alikuwa ni mwanaisimu wa kwanza kupendekeza mpangilio wa lugha kwa kuainisha lugha 30 mbalimbali za Uropa, Afrika, Asia, Wamerikani Asilia na Osenia. Baadhi ya lugha za Kiafrika zilizojumlishwa ni kama vile Kiswahili, Kipulaa, na Kimasaai miongoni mwa zingine. Alisisitiza sana upangaji wa lugha za Kiafrika kwa kupendekeza kanuni bia 45 zinazotumika kuainisha lugha hizo kimuundo. Greenberg anaeleza kuwa aliteua sampuli/ lugha hizi kwa upana ili kupata matokeo ya kutosheleza utafiti wake. Anaendelea kueleza kuwa kwa kiwango kikubwa matokeo yake yapaswa kuwa kamilifu kwa kiwango cha juu katika kuchanganua miundo ya lugha zote. Kwa hivyo, kanuni hizi yapaswa kuwa halali. Kanuni alizotumia kuainisha lugha hizi zina vigezo vitatu kama vile: uwepo wa vihusishi vya kabla ya nomino dhidi ya vihusishi vya baada ya nomino, mpangilio wa nomino na kitenzi, na yambwa katika lugha mbalimbali.

Baadhi ya kanuni bia za Greenberg zilizotumika ni zile ambazo zililenga kuchangia madhumuni ya utafiti huu kwa kuchunguza muundo wa vihusishi vya Kiswahili ili kubainisha iwapo kuna ukiukaji unavyojitokeza, yaani zile zinazozungumzia vihusishi peke yake. Kwa hivyo, kutokana na hivyo vigezo vitatu, kigezo cha uwepo wa vihusishi vya kabla ya nomino dhidi ya vihusishi vya baada ya nomino ndicho kilichotumika hivi kwamba, kanuni nyinginezo hazikutajwa hapa kwa kuwa zinahusu kategoria nyingine za maneno na hivyo basi haziwezi kuchangia utafiti huu ambao unalenga vihusishi na virai vihusishi. Hata hivyo, kanuni za uchanganuzi zitatajwa katika sehemu ya mwisho uchambuzi wao utakapoonyeshwa. Kanuni bia inabeba sifa bia za lugha kama anavyoeleza Hockett (1961). Anaeleza kuwa kanuni bia za lugha ni sifa zinazotumika katika idadi kubwa ya lugha ulimwenguni. Madai haya yanachukulia kanuni bia kama nadharia ya kuchunguza muundo wa lugha. Hatuwezi kuunda kanuni bia za lugha, ila tunapaswa kuzigundua hata kama jambo hili si kawaida na rahisi. Bloomfield (1933) anaeleza kuwa njia muhimu ya kuchukulia kuwa kanuni bia hutumika kwa lugha zote, ni utafiti na uchambuzi wa lugha hizo. Kanuni bia za lugha ni urasimu unaokuwa na maumbo au miundo ya sarufi zote za lugha kama vile sifa, aina za sheria na kadhalika. Kwa jumla, kanuni bia zinaweza kueleweka kama kauli jumuishi zinazomilikiwa na lugha zote au idadi kubwa ya lugha hizo kama zinavyojidhihirisha kwa lugha husika. Kanuni bia ni muhimu sana katika kushughulikia taipolojia ya lugha.

Taipolojia ya lugha ni uwanja ambao unachunguza na kuainisha lugha kulingana na muundo na dhima ya vipashio vyake, kusudi lake likiwa ni kueleza kufanana na kutofautiana kwa lugha mbalimbali ulimwenguni. Greenberg (1963) anaeleza kuwa taipolojia inaazimia kuleta maafikiano yanayotarajiwa katika lugha. Hata ingawa hatutapinga kuwa kuna sifa ambazo zinaafikiana kwa lugha zote, kielelezo hiki hulenga kimsingi kuchambua namna ambapo lugha mbalimbali hutofautiana na kanuni zinazoiongoza. Lugha tarajiwa ya mwanadamu ni

ile ambayo sifa zake hupatikana katika misingi ya vigezo vinavyokubalika na utofauti unaotumika kueleza na kuchambua lugha. Kwa kauli hii ile lugha isiyoweza kuelezeka basi haiwezi kutarajiwa kuwa lugha ya binadamu. Uainishaji wa lugha zinazoundwa kutokana na misingi na sifa zinazotajwa kwa kanuni zinazoonyesha utofauti na kuweza kueleza ndizo huchukuliwa kuwa taipolojia. Keenan (1978) anasema kuwa kanuni bia ni uelezaji wa sifa za utaratibu kwa njia ambayo lugha hutofautiana kutoka kwa nyingine katika taipolojia. Miundo inayotofautiana ni jambo la kimsingi litakaloangaziwa. Katika utafiti huu tutazingatia mwanaisimu mmoja tu aliyetafiti kanuni bia za mpangilio wa maneno ya lugha mbalimbali ambaye ni Greenberg (1963).

Utendakazi wa kanuni hizi ni wa kihusiano hivi kwamba ikiwa lugha fulani ina sifa A basi lazima ina sifa ya B. Greenberg alipendekeza kanuni bia hizi kwa mtazamo wake aidha kwa takwimu alizokusanya au kuwa na uhakika kabisa kuwa lugha fulani ina sifa fulani. Kanuni bia hizi zilipendekezwa kwa kuzingatia sifa fulani ya kusema kuwa ikiwa lugha ina sifa A basi lazima matokeo ya sifa B yawepo na kinyume chake. Uwepo wa sifa A kujitokeza na sifa B kukosa kujitokeza huleta ukiushi wa lugha hiyo maana sifa A na B zinafaa kuwepo kwa pamoja katika lugha hiyo. Lakini kwa mtazamo unaoweza kujitokeza ni kwamba lugha inaweza kuwa na sifa A bila sifa B au ikatokea kwamba hamna sifa A wala sifa B. Na hii ndiyo kauli muhimu tutakayozingatia katika uhakiki wa kanuni hizi. Ikiwa matokeo ya mwisho ya kauli hii yatajitokeza basi kanuni hiyo itakuwa imekiukwa na lugha hii. Swali linaloibuka ni je, kanuni bia za Greenberg zimefanikiwaje katika kueleza data ya lugha zote alizozitumia?

Greenberg (1963), anaeleza katika utangulizi kuwa kanuni bia alizotaja haziwezi kukumbatiwa na lugha zote ulimwenguni maana hata katika utafiti wake hakuweza kuzichambua lugha zote na hizi alizozitaja si kanuni pekee zinazoruhusiwa kuchambua lugha, huenda kuna zingine nyingi kulingana na elementi za lugha. Greenberg alidhamiria kueleza kuwa kwa kiwango kikubwa

matokeo ya utafiti wake yapaswa kuwa kamilifu/ kukubalika kwa kiwango kikubwa au yawe ya ukweli/ halali katika uchanganuzi wa miundo ya lugha zote. Kwa hivyo aliacha asilimia chache mno ya ughairi lakini vinginevyo anaamini kuwa kanuni hizi zinapaswa kukubalika bila kizuizi na lugha hizi.

Kwa ujumla, Greenberg (1963) anaeleza kuwa lugha fulani huwa na mazoea ya mara kwa mara katika kubadili au kuzuia elementi kabla ya vivumishi au vizuizi ilhali zingine hufanya kinyume. Kwa mfano, Greenberg anaeleza kuwa lugha zingine huwa na mazoea ya kuvumisha elementi kabla ya vivumishi, ilhali lugha zingine hufanya kinyume. Kwa mfano, lugha zingine kama Kituruki huweka vivumishi kabla ya nomino vinavyovumisha, pia huweka yambwa tendwa kabla ya kitenzi, kimilikishi cha binafsi kabla ya nomino, na kielezi kabla ya kivumishi kinachovumisha. Lugha kama hizi, hata hivyo, huwa na mazoea ya kuwa na vihusishi vinavyokuja baada ya nomino vinavyoelezwa na misamiati ya Kingereza. Lugha yenye kinyume ni ya Thai ambayo vivumishi vyake hufuata nomino, na yambwa hufuata kitenzi, kimilikishi hufuata nomino tawala na huwa na vihusishi vya kabla ya nomino. Katika lugha ya Kiingereza, kuna vihusishi vya kabla ya nomino, na yambwa tendwa hufuata kitenzi. Kwa upande mwingine, Kingereza na lugha ya Kituruki hufanana kwa vivumishi vinavyotangulia nomino. Hata hivyo, tungo za vimilikishi hujitokeza. Katika lugha alizoeleza Greenberg, 14 zinamiliki vihusishi vinavyokuja baada ya nomino na katika kila lugha, mpangilio wa umilikishi unachukua vimilikishi vinavyofuatwa na nomino tawala. Lugha 13 katika hizi 14 huwa na kimilikishi kinachofuata nomino tawala. Lugha moja tu ndiyo haikubali mpangilio huu na hivyo basi kufikia madai ya kanuni hii ya pili. Katika maelezo yake, Greenberg hajaeleza wala kuchambua lugha hizi moja kwa moja kwa kutoa data iliyo wazi. Kuno (1974), anazungumza kwa kina kuhusu mpangilio huu. Katika kumnukuu Greenberg, Kuno anataja kanuni zingine zinazochukua mpangilio huu kwa njia mbalimbali za ujenzi wa kazi yao. Kanuni ya nne, kumi na mbili, kumi na sita, kumi na saba na

ishirini na nne zimeangaziwa kwa mtajo. Greenberg aliweza kutaja kanuni hizi bila kutoa maelezo au uchambuzi wa kueleza kuwepo kwa madai yake katika lugha. Kwa hivyo, Kuno anajaribu kujibu baadhi ya maswali yanayoibuka katika lugha zinazokumbatia kanuni hizi. Katika utafiti wake aliweza kuteua lugha za sehemu mbalimbali kama vile Uropa, Asia, Wamerekani Asilia, Osenia na Afrika. Katika lugha za Kiafrika, Kiswahili kilikuwa mojawapo ya zile zilizotumika kama data yake. Na hili linatuelekeza kwa sehemu yetu ya kuchunguza iwapo baadhi ya kanuni bia hizi zinadhihirika au zinakiukwa na lugha hii.

YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Tafiti kadhaa zimefanywa na wataalamu wengi kuhusu vihusishi kwa kuzingatia malengo mbalimbali ya vihusishi katika lugha mbalimbali. Baadhi ya wataalamu hawa wametoa madai yafuatayo

Koopman (2000) akiandika kuhusu lugha ya Kiholanzi, anaeleza kuwa vihusishi vingi huwekwa kabla ya nomino au baada ya nomino. Hata hivyo vihusishi vya kabla ya nomino na baada ya nomino vyaweza kutumika vyote katika sentensi moja. Koopman amefanya utafiti wake huku akichunguza mchango wa kisemantiki wa Kiholanzi kwa kulinganisha vihusishi hivi vya kabla na baada ya nomino. Pia ameeleza usanifu wa vihusishi vilivyomo kwa modeli ya sintaksia. Utafiti wa Koopman umechangia katika kueleza muundo wa vihusishi vya lugha ya Kiholanzi. Hivyo basi utafiti wa Koopman ulikuwa wa manufaa kwa utafiti wetu kwa sababu amechanganua muundo wa vihusishi, jambo ambalo linashabihiana na mada yetu hata ingawa lugha aliyoitafitia ni tofauti na ile tuliyoitumia. Kiswahili kinamiliki vihusishi vya kabla ya nomino na baada ya nomino. Tofauti kati ya utafiti wa Koopman na utafiti wetu ni kwamba, alichunguza vihusishi kisemantiki, utafiti huu ulichanganuliwa kisintaksia na wala si kisemantiki.

Huddleston (2000) anaeleza kuwa sehemu ya vihusishi kulingana na uhusiano wake wa kijalizo

katika lugha fulani, kwa kawaida huwa na uhusiano wa vipengele fulani katika mfuatano wa elementi za lugha hiyo. Alishikilia kuwa hii ndiyo sababu utapata kuwa vihusishi vya lugha zenye utaratibu wa kiima- kitenzi- yambwa kama Kiingereza hufuata kijalizo. Tofauti na haya, lugha zingine kama vile Kijapani zenye muundo wa kiima- yambwa –kitenzi, vitenzi hufuata vijalizo sawa na vihusishi. Kufuatia mtazamo huu wa Huddleston, utafiti wetu kwa kiwango fulani uliangazia mahusiano ya vihusishi na maneno mengine katika muktadha wa sentensi.

Lefebvre na Brousscau (2001) walifanya utafiti katika lugha ya Fongbe. Wanaeleza kuwa vihusishi vya kabla ya nomino vilionekana kuwa na uhusiano wa vipindi mbalimbali vya kihistoria (daikronia). Vihusishi hubadilika kihistoria na vinahusiana na nomino kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, tofauti wa maneno yenye maana tofauti lakini inayokaribiana hujitokeza. Lugha iliyozingatiwa hapa ni tofauti na ile lugha tuliyoitafitia. Tulitafiti lugha ya Kiswahili na wala si Fongbe. Utafiti wetu haukuangazia historia wala kueleza jinsi uwekaji wa vihusishi visivyo vya asili vilivyozuka. Hata hivyo, utafiti wetu ulirejelea vihusishi vya kabla ya nomino mara kadhaa, kwa hivyo utafiti huu ni wa manufaa sana.

Hopper na Traugott (2003) wanaeleza kuwa kuna kategoria mbili za vihusishi wanapozingatia kiwango cha kisemantiki. Wanaeleza kuwa kategoria ya kwanza ni vihusishi vya kimsingi. Hivi ni vihusishi ambavyo hutangulia kwa idadi kubwa ya wazungumzaji wa lugha. Wanaendelea kueleza kuwa katika lugha yenye virai vihusishi, vihusishi vya kabla ya nomino huwa vinatofautiana na vihusishi vya baada ya nomino kwa kiwango cha semantiki dhahania. Beliavsky (2004) naye anaeleza kuwa katika udhahania wa vihusishi, vihusishi dhahania vinapotumika zaidi, ndivyo vinapotawala kisintaksia na kinyume. Katika kufafanua swala hii. Tyler na Evans (2003) wanaeleza kuwa ni bora ikiwa tutachukulia kuwa, katika vipindi vya mwanzo wa historia ya maneno, maana ilikuwa finyu. Kwa mfano, kihusishi juu ya kilikuwa na maana moja asili. Lakini sasa hivi maneno yamepewa maana kadhaa

ambayo wakati mwingine huwa ni ya kudhania tu. Wanaendelea kufafanua kauli hiyo kwa kuuliza swali kwamba, iweje mzungumzaji akachagua kutumia kihusishi fulani kwa njia isiyo ya kiasili, aidha bila kukibadilisha kifonolojia lakini msikilizaji akaelewa maana kwa kuidhania kuwa huenda ndiyo msemaji aliikusudia? Katika utafiti huu vihusishi vimechanganuliwa kwa misingi ya kisemantiki ili kubainisha maana asili na maana isiyo asili kadri wakati unavyozidi kusonga. Hili ni tofauti na utafiti wetu lakini utafiti wenyewe bado ni wa manufaa makubwa. Vihusishi vya kabla ya nomino na baada ya nomino viliangaziwa katika utafiti wetu na hivyo kufanikisha lengo letu la utafiti.

MATOKEO YA UTAFITI

Sehemu hii, inachanganua kila kanuni inayohusu uwekaji wa vihusishi ili kuchunguza iwapo Kiswahili kinaghairi au kinatii kanuni husika.

Kanuni ya 2: Kimilikishi na Nomino

Katika lugha zenye vihusishi vinavyojitokeza kabla ya nomino, angalau kimilikishi hufuata nomino inayovitawala, ilhali katika lugha zenye vihusishi vinavyojitokeza baada ya nomino aghalabu vimilikishi vyake hutangulia nomino.

Kiswahili ni lugha yenye vihusishi vinavyokuja kabla na baada ya nomino. Kanuni hii inafuatwa, tutaangazia mifano mbalimbali ya vimilikishi vya Kiswahili na jinsi vinajitokeza katika sentensi. Tutazingatia vimilikishi vya nafsi na vimilikishi vya –a unganifu.

Vimilikishi vya Kiswahili hutegemea hali mbili: nafsi na ngeli ya nomino. Lugha ya Kiswahili ina nafsi tatu, ya kwanza, ya pili na ya tatu zinazochukua hali ya umoja na wingi. Nomino zinapoambishwa kwa kuwekwa viambishi awali basi makundi ya ngeli huwa yametambulishwa. Hatutaingilia sana swala na ngeli ila tutaonyesha jinsi nafsi na baadhi ya ngeli hutumika kwa lugha ya Kiswahili.

Maelezo ya kina yanaweza kuonekana katika mifano hii:

- a) Mtoto aliingia kwa nyumba yake na kulala.
- b) Watoto waliingia kwa vyumba vyao na kulala.

Katika mfano huu, yake ni kivumishi kimilikishi kinachotumika kuonyesha kuwa nomino inamiliki nyingine. Mizizi ya vivumishi vimilikishi huundwa kulingana na nafsi mbalimbali kama vile-angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao. Katika sentensi (1), kimilikishi yake na vyao vinafuata nomino nyumba Vilevile kimilikishi kinaweza kuambishwa na nomino tawala ifuatavyo:

- Ninampenda mamangu sana.

Katika sentensi ya (2) silabi ya mwisho ndiyo kimilikishi na hivyo imeunganishwa na nomino tawala kutoka kwa tokeo la; mama + yangu = mamangu. Yangu ni kimilikishi na silabi ya mwisho imeunganishwa kutokana na michakato ya mofonolojia au mofosintaksia na kimilikishi hiki huambishwa na kufuata nomino tawala.

Viimilikishi vya –a unganifu hutumika kuonyesha uhusiano na umilikaji, kwa mfano:

- a) Nyumba ya baba imeungua.

Katika mfano huu, ya ni kivumishi ambacho hutumika kuonyesha uhusiano na umilikaji. Kinaitwa kimilikishi cha –a unganifu. Vimilikishi vya –a unganifu vinaweza kutumika katika muktadha mwingine kama vihusishi. Nomino tawala ya kivumishi kimilikishi kimetangulia nomino tawala ambacho ni nyumba. Kutokana na mfano wa sehemu hii, lugha ya Kiswahili ina vimilikishi vinavyofuata nomino tawala na hili linatii sifa ya kwanza ya kanuni hii inayoeleza kuwa katika lugha zenye vihusishi vinavyojitokeza kabla ya nomino, angalau kimilikishi hufuata nomino inayovitawala. Ukiukaji unaonekana katika sehemu ya pili ya kanuni hii. Tukirejelea mantiki inayozingatiwa katika uchanganuzi wa kanuni bia hizi kwamba, ikiwa lugha ina sifa A katika mpangilio wa maneno, basi itakuwa na sifa B, lugha hii ya Kiswahili imeonyesha utifuu wa kuwa na sifa A lakini imekiuka sifa B tukijikita katika mpangilio wa maneno pekee. Isitoshe, tunapofasili

kiambishi -ni ambacho kinaambishwa mwishoni mwa nomino tutaona kuwa Kiswahili kina vihusishi vya baada ya nomino. Haya yanadhihirisha ukiushi wa kanuni hii ya Greenberg.

Kwa mujibu wa Greenberg (1963), kimilikishi hufuata nomino tawala kwa lugha zenye vihusishi vinavyokuja kabla ya nomino. Katika lugha zenye vihusishi vinavyokuja baada ya nomino huwa na vimilikishi vinavyotangulia nomino. Dryer (1991) anadokeza kuwa lugha zote alizotumia Greenberg kufanya utafiti wake haziambatani na matokeo kwa sababu hakuwa na data ya kutosha kwa lugha hizo na vilevile anaeleza kuwa Greenberg hakutoa data iliyochambuliwa ya lugha hizi moja kwa moja.

Kanuni ya 3: Mpangilio wa Kitenzi-Kiima-Yambwa

Lugha zenye mpangilio wa kitenzi + kiima + yambwa huwa na vihusishi vya kabla ya nomino.

Katika sentensi sahili za Kiswahili, mpangilio wa maneno huwa wa Kiima-Kitenzi-Yambwa kama inavyoonyeshwa katika mfano wa 4a.

- a) Fatima amelima shamba.
- b) Shamba lilimwa na Fatima.
- c) Amelima shamba.

Katika mfano huu wa (4a) ‘Fatuma’ ni kiima, ‘amelima’ ni kitenzi na yambwa ni ‘shamba’. Kiswahili kina vihusishi vya kabla ya nomino, lakini muundo wa sentensi sahili si kitenzi – kiima – yambwa. Hata hivyo, lugha ya Kiswahili huruhusu uhamaji wa vipengele vya sentensi kutoka sehemu moja hadi nyingine kama ilivyoangaziwa katika sura ya tatu. Katika sentensi ya (4b) shamba ni yambwa, lilimwa ni kitenzi na Fatima ndiye kiima kilichotenda jambo. Mpangilio huu umeonekana kuwa (yambwa- kitenzi-kiima). Kiswahili hakijaruhusu kauli hii kuchukuliwa kama mpangilio mbadala wa lugha hii kwa sababu kuna mifanyiko ya kisintaksia ambayo imefanyika na kusababisha michakato ya uhamishaji unaonekana hapa. Utata unaonekana

kwa sababu kitenzi kina uhuru wa kunyambuliwa na hivyo kurejelea mpangilio wa (4c) ambao unaweza kufanya ione kama Kiswahili kinaruhusu mpangilio wa kitenzi – yambwa. Hata hivyo, maana inabaki kuwa ile ile, yaani mpangilio wa kiima – kitenzi - yambwa kupewa usukani kwa sababu kiambishi awali a-kinarejelea kiima. Ingawa maneno yanayoonekana ni kitenzi na yambwa, sehemu ya kiima ni kapa, lakini bado inashiriki katika michakato ya kimfosintaksia. Hii ndiyo sababu kiambishi awali a- katika amelima shamba kinaafikiana na kiima kapa. Ili kuyakinisha kuwepo kwa vihusishi vya kabla ya nomino katika lugha ya Kiswahili kufuatia madai ya kanuni 3 ya Greenberg, muundo wa sentensi (4a) unafaa kuwa kama wa 5.

- *Amelima Fatuma shamba.

Katika mfano huu ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili haitakubali mpangilio huu. Ukiukaji unajitokeza katika kanuni hii ya tatu kwa sababu hakuna mpangilio wa kitenzi- kiima- yambwa katika lugha ya Kiswahili. Licha ya hayo, lugha hii inamiliki mpangilio wa vihusishi vya kabla ya nomino.

Kanuni ya 4: Muundo wa Kiima-Yambwa-Kitenzi

Lugha za kawaida zilizo na muundo wa Kiima-Yambwa- Kitenzi angalau huwa na vihusishi vinavyojitokeza baada ya nomino.

Kufuatilia maelezo ya kanuni ya tatu ambayo yamejadiliwa hapo mwanzo, kanuni hii ya nne pia inaonekana kuchukua mkondo tofauti na mpangilio wa kawaida wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili inaweza kuambisha vipatanishi vya yambwa kwenye kirai kitenzi kabla ya mzizi wa kitenzi na vipatanishi hivi vinaweza kuwa vya yambwa tendwa au tendewa kulingana na muundo wa sentensi husika. Kiswahili kikiwa lugha ambishi bainishi wakati mwingine huambisha kipatanishi cha yambwa katika kitenzi kama vile: Fatuma amemlimia Ali shamba.

Kwa mfano:

- a) Aliwapikia chakula.
- b) Sakaja amemtupia mpira.

Katika mifano ya (6ab) viambishi wa na m ni viambishi vya yambwa tendewa vinavyotangulia mzizi wa kitenzi. Ikiwa itazingatiwa kama mpangilio mbadala wa kiima – yambwa – kitenzi huku Halima/Sakaja zikiainishwa kama kiima na wa/m kuainishwa kama yambwa tendewa na chakula/mpira yambwa tendwa basi lugha hii itachukuliwa kuwa inatii kanuni ya nne. Ughairi unatokea wakati ambapo lugha ya Kiswahili inatambulika kwa mpangilio mmoja tu wa maneno wa Kiima-Kitenzi-yambwa kama mpangilio mkuu. Vilevile, kuweko kwa yambwa tendwa katika mifano hii kunaendelea kuleta utata katika ufasiri wa kanuni hii.

Kanuni ya 9: Vishirikishi vya Maswali na Viambishi vya Maswali

Ikiwa uwezekano wa mara kwa mara hutokea, wakati vishirikishi vya maswali na viambishi vinapoambishwa kwa sehemu nzima ya sentensi na kuirejelea, ikiwa ni vya mwanzo, basi elementi hizo hupatikana katika lugha zenye vihusishi vya kabla ya nomino. Ikiwa ni vya mwisho, basi hupatikana kwa lugha zenye vihusishi vya baada ya nomino.

Greenberg (1963) anaeleza kuwa vishirikishi vya maswali au viambishi, vinapodhihirishwa katika nafasi ya urejeshi kwa neno katika tungo, huwa vinafuata neno hilo. Vishirikishi hivyo havijitokezi kwa lugha zenye muundo tawala wenye mpangilio wa Kitenzi- Kiima- Yambwa. Kanuni hii ni ya kiujumlishi na inachukulia kuwa kila lugha ina vipashio vinavyobainisha maswali. Hata hivyo, baadhi ya lugha huwa na mbinu mbadala za kuuliza maswali. Katika lugha ya Kiswahili, si lazima kuwe na vishirikishi vya maswali au viambishi vinavyorejelea swali. Katika sentensi zenye maswali ya ndio/la kwa mfano, kiimbo hutumika kama muundo mbadala.

Vilevile, lugha ya Kiswahili huwa na vishirikishi vya maswali vinavyojitokeza katika sehemu mbalimbali. Vishirikishi vya mwanzoni huanza na je, kwa nini, mbona n.k. Kwa mfano:

- Je, funguo zipi zilizopotea?

b) Kwa nini ulizipoteza funguo?

Katika (7) je, na kwa nini ni vishirikishi vya maswali vinavyotokea mwanzoni mwa sentensi. Aina nyingine ya vishirikishi ni vile vinavyoambishwa na ngeli kama vile –ngapi, -ipi na kadhalika ambavyo ni vivumishi viulizi. Tazama mfano:

- a) Walifika wangapi?

b) Funguo zipi zilipotea?

Vishirikishi hivi –ngapi na –ipi vimeambishwa viambishi vya ngeli (wa-, z-). Lugha ya Kiswahili huwa na mifano mingi ya vishirikishi vinavyoundwa kwa namna hii. Isitoshe, kuna vishirikishi vingine vinavyotumika mwishoni mwa sentensi swali linapotokea kama vile, je, lipi n.k. Kwa mfano:

- a) Babu ameangukaje?

b) Anatomia gari lipi?

Vishirikishi hivi hunuia kujua hali ya jambo lilivyotokea. Kuna vishirikishi kadha vya maswali ambavyo hutumika katika lugha ya Kiswahili na vingi vyavyo hulingana na jinsi vinapotumika katika muktadha kwa maana kuna vile ambavyo vinaweza kutumika katikati au mwanzoni pamoja na ngapi, vingapi, mingapi, wangapi, ipi (yupi, yapi, kipi, upi), kwa nini, nani, wapi, nini na gani. Yanayojitokeza katika sehemu hii ni kwamba, kuna uwezekano wa mara kwa mara wa vishirikishi vya maswali na viambishi kutokea mwanzoni mwa sentensi na mwishoni vilevile. Lugha ya Kiswahili imetii kanuni hii kwa sababu ina vihusishi vya kabla na baada ya nomino.

Licha ya Kiswahili kutii kanuni hii, tatizo ni kuwa kanuni hii inashughulikia lugha mbili, lugha inayokuwa na vishirikishi vya maswali mwanzoni na lugha nyingine ambayo huwa na vishirikishi vya maswali mwishoni. Kutokana na kuwa Kiswahili kina vishirikishi mwanzoni na mwishoni na- pia kuna miundo ya maswali bila vishirikishi basi, kanuni hii inakosa uwazi

tunapokuja kwa Kiswahili. Upana wa ufasiri huu unafanya iwe vigumu kukiweka Kiswahili kikundi kimoja na kingine.

Kanuni ya 22: Ulinganishi

Ikiwa katika ulinganishaji bora mpangilio wa kipekee au mbadala ni kilinganishwa-kilinganishi- kivumishi basi lugha hiyo ni ya vihusishi vinavyokuja baada ya nomino. Iwapo muundo wa ulinganishaji unaozidi kujitokeza kila mara ni kivumishi- kilinganishi- kilinganishwa basi lugha hiyo ni ya vihusishi vya kabla ya nomino.

Greenberg (1963) anaeleza kuhusu vivumishi hasa vile vya kulinganisha vinavyoonyesha ubora wa kitu kwa kingine. Lugha chache mno ulimwenguni kama vile Kingereza hurejelea ulinganishaji wa miundo ya vivumishi kulingana na maoni yake. Lugha ya Kiswahili vilevile inamiliki ulinganishi. Katika maelezo ya Greenberg (1966), kuna elementi tatu ambazo anatarajia kuwa mpangilio unapaswa kuzingatia kwa mfano:

- a) Alice ni mrefu kuliko John.

b) Halima ni bora kama Hamisi.

Maneno yaliyokolezwa ndiyo huitwa kivumishi, kilinganishi, kilinganishwa. Utaratibu unaohitajika hapa ni ule wa kuwa na kivumishi, neno la kulinganisha, na kinacholinganishwa au kinyume chake. Vilinganishi hivi ni pamoja na; kuliko, zaidi ya, kama, mithili ya n.k. Katika mifano ifutayo, tutatazama iwapo Kiswahili kinadhahirisha mpangilio huu.

a) Emma ni mrembo zaidi kuliko Abigael.

b) Elihu huyu ni mtiifu zaidi ya mbwa yule.

Kiswahili kina mifano mingi ya ulinganishi na inavyoonekana hapo juu, lugha hii inachukua mpangilio wa kilinganishwa-kivumishi-kilinganishi. Katika sentensi ya (10a, b), Emma/Elihu ni kilinganishwa, mrembo/mtiifu ni kivumishi na kuliko ndicho kilinganishi. Kutokana na mifano iliyoorodheshwa katika (10),

inadhihirika kwamba kivumishi hufuata nomino inayolinganishwa na kivumishi hutangulia kilinganishi. Ulinganishaji unapotokea, lazima kuwepo na nomino mbili au vitu viwili na kimoja hushinda kingine kwa kuwa na sifa inayozidi hiyo nomino nyingine. Sentensi ya (10a) urembo wa Emma unatumika kulinganisha ule wa Abigael. Mrembo zaidi ni kivumishi cha sifa na kivumishi hutumika kuvumisha au kutoa sifa zaidi kuhusu nomino inayokitangulia, Emma ni nomino linganishwa na Abigael ni kilinganishwa. Kulingana na maelezo haya, inaoonekana kuwa lugha hii haijazingatia mpangilio wa ulinganishi uliopendekezwa na Greenberg katika kanuni hii na hivyo kuturuhusu kuhitimisha kuwa kuna ukiukaji katika sehemu zote mbili hata ingawa ni lugha ya vihusishi vya baada ya nomino na kabla ya nomino.

Kanuni ya 24: Usemi Rejeshi

Ikiwa neno/usemi rejeshi utatangulia nomino aidha ukawa muundo wa kipekee au muundo mbadala, basi huenda lugha hiyo ikawa ya vihusishi vya baada ya nomino au kivumishi chake hutangulia nomino au zote.

Katika kanuni hii, Greenberg anaelezea kishazi rejeshi kinachovumisha nomino kwa mfano; mimi nilimwona mtoto aliyelia. Katika sentensi hii, aliyelia ndilo neno rejeshi na katika sentensi hii, linatokea baada ya nomino mtoto.

Greenberg (1963) anaendelea kueleza kuwa ni lugha moja tu ambayo si ya kawaida kati ya zile alizotafiti ambayo kihusishi chake hutangulia nomino, Kichina ambayo vihusishi vyake hutangulia nomino licha ya kuwa neno rejeshi hutangulia nomino. Katika mpangilio wa kivumishi- nomino, kama ilivyo katika kishazi cha Kingereza ‘my book’ mwelekeo wa kawaida ni neno rejeshi kufuata nomino linalorejelea.

Lugha ya Kiswahili ina virejeshi vya amba- na -o rejeshi. Amba- hutumika katika sarufi katika kukirejesha kitendo kwa jina lililotajwa na ndipo mofimu hii yaweza kuitwa kiwakilishi kirejeshi. Mifano ya (11) inaonyesha matumizi ya kirejeshi amba-;

- a) Maembe makubwa ambayo yameiva ni hayo.

b) Mahali pazuri ambapo alitoka ni hapa.

Amba- imetumika kurejesha ‘yameiva’ kwa ‘maembe’ na ‘alitoka’ kwa ‘mahali’. Mofimu hii ya amba- huwa inabadilikabadilika katika sentensi kulingana na ngeli iliyotumiwa. Katika kanuni hii, Greenberg anaeleza juu ya mpangilio wa kivumishi ili kuhakiki sifa zote mbili, mifano ya (11b) inaonyesha kwamba, kivumishi kinafuata nomino katika sentensi. Ni muhimu kutaja hapa kuwa mzizi neno –amba la urejeshi katika Kiswahili huainishwa kama kivumishi. Haya yanatokana na kuwa neno la urejeshi hutoa maelezo kuhusu nomino husika. Kutokana na haya, ni kawaida kuwa neno rejeshi litafuata muundo wa Kiswahili ambao kivumishi hufuata nomino.

Kirejeshi cha o- kinaweza kutumika katika kitenzi ili kukipa maana ya kuhusiana. Katika matumizi haya, kinaweza kuja katikati au kutumika mwishoni. Kwa mfano:

- a) Mwanafunzi yeyote anayetia bidii hufaulu.
- b) Nguo yoyote ichafukayo hufuliwa tena.

Mifano ya (12a,b) inaonyesha kuwa kiambishi tamati cha urejeshi kinaambishwa kabla ya mzizi wa kitenzi au mwishoni wa kitenzi. Kiambishi hicho kinawiana na kivumishi cha pekee ambacho kwa upande wake kinawiana na ngeli ya nomino kinayovumisha. Kitenzi kilichoambishwa kiambishi tamati cha urejeshi kinabadilika na kuwa kiwakilishi cha urejeshi ambacho pia ni aina nyingine ya kivumishi. Hivyo basi sentensi ya (12a,b) zinaonyesha nomino ambayo inafuatwa na vivumishi viwili.

Katika kufasili muundo huu wa Kiswahili kwa mujibu wa kanuni 24 ya Greenberg kuwa lugha ambayo neno rejeshi hutangulia kivumishi huwa na vihusishi vya baada ya nomino. Kiswahili kinaonekana kutii kanuni hii kwamba maneno rejeshi hufuata nomino na hivyo kuifanya lugha yenye vihusishi vya kabla ya nomino. Hata hivyo, kulingana na fasili yetu, tulionyesha kuwa kuna

baadhi ya mipangilio ya maneno ambapo vihusishi vinajitokeza baada ya nomino kwa mujibu wa mkabala wa kimapokeo na pia katika kategoria fulani za virai. Kwa kauli hiyo basi, kanuni hii itasemekana kukiukwa.

Kanuni ya 27: Viambishi Tamati na Viambishi Awali

Lugha zinazongezewa viambishi tamati bila shaka ni lugha zenye vihusishi vinavyojitokeza baada ya nomino, na ikiwa viambishi vya awali vinaongezwa, basi lugha hiyo huchukua muundo wa vihusishi vya kabla ya nomino.

Katika maelezo ya mwanzo ya sehemu hii, Greenberg (1966) anaeleza sehemu ya mwisho ya kanuni hizi huku akirejelea mofimu na mifanyiko yake. Unyambulishaji au uundaji wa maneno mapya kutokana na vina na mashina, unyambulishaji wa majina, vitenzi n.k na unyambulisho wa maneno ni elementi ambazo zimewekwa katika kundi moja kuu la viambishi. Kulingana na mpangilio wavyo kwa kuzingatia shina/ mzizi wa neno, viambishi vimegawanywa katika sehemu mbili: viambishi awali na viambishi tamati. Anaendelea kueleza kuwa lugha zenye viambishi tamati huwa nyingi ikilinganishwa na lugha za viambishi awali ambazo ni chache mno. Greenberg anaeleza kuwa katika hizi lugha 30 ni lugha ya Thai tu ambayo huonekana kuwa ya viambishi awali pekee. Kanuni ya Greenberg inajikita katika kugawanya lugha katika makundi mawili: i) lugha zenye viambishi awali pekee na lugha zenye viambishi tamati pekee. Tatizo kubwa ni kuwa baadhi ya lugha zinaweza kuwa na viambishi awali na viambishi tamati. Tutachunguza jinsi kanuni hii inavyodhihirika katika lugha ya Kiswahili.

Kiswahili ni lugha ambishi bainishi yenye viambishi tamati na viambishi awali. Viambishi awali na viambishi tamati katika uambishaji wa nomino vimeonyeshwa katika mifano 13 na 14.

- a) M-shambulia-ji
- b) Ma-ony-esho-o

Viambishi awali na tamati katika vitenzi ni kama vile:

14. Wa-li-o-pig-ana-a

b) A-li-m-tambu-a

Tumeonyesha jinsi uambishaji unaweza kutokea katika maneno ya lugha ya Kiswahili ambapo nomino na vitenzi humiliki viambishi awali na viambishi tamati. Katika kanuni hii ya Greenberg ya (27), amegawa kanuni hii katika makundi mawili ya lugha mbili. Kigezo cha kiambishi awali na kiambishi tamati kinazua changamoto katika kuainisha Kiswahili kama lugha ya vihusishi vya kabla ya nomino au vihusishi vya baada ya nomino kwa sababu ina viambishi awali na pia viambishi tamati, Hivyo basi, kwa upande mmoja, tunaweza kudai kuwa kanuni hii ya Greenberg imefaulu kwa sababu kuweco kwa viambishi tamati kunaifanya itimize sharti la kuwa na vihusishi vya kabla ya nomino. Vilevile, kuwepo kwa viambishi tamati kunaifanya itimize sharti ya vivumishi vya baada ya nomino. Kwa upande mwingine, utata unaingia ikiwa lugha hii inatii kanuni hii au inakiuka kwa sababu Greenberg hakueleza kuwa lugha moja inaweza kuwa na sifa zote mbili za sehemu ya kwanza ya lugha zenye vihusishi vya kabla ya nomino na sehemu ya pili ya vihusishi vya baada ya nomino. Tatizo ni kuwa tukiwa na kanuni ambayo haiwezi kutofautisha lugha moja na nyingine, basi kanuni hiyo haiwezi kusaidia katika ubainishaji wa taipolojia ya lugha.

Kutatua Tatizo la Kitaipolojia

Imebainika wazi kwamba baadhi ya kanuni hizi au sehemu moja ya kanuni hizi zinakubalika na lugha ya Kiswahili ijapokuwa kuna kanuni zingine ambazo zinakiukwa. Utafiti wetu ulidhamiria kuhakiki iwapo lugha ya Kiswahili inatii kanuni hizi kuhusu vihusishi kwa kuzingatia kuwa lugha hii ilikuwa mojawapo ya data za Greenberg katika utafiti na imebainika kwamba sehemu kubwa ya kanuni hizi zinakiukwa. Baadhi ya kanuni zina utata ambao unafanya juhudi za kutoa kauli jumlishi kuwa na changamoto. Kutokana na uchambuzi wetu, ni wazi kuwa kutegemea

muundo nje wa mpangilio wa maneno kufuata mkabala wa sarufi mapokeo hakuwezi kutusaidia katika kuyakinisha madai muhimu ya taipolojia ya lugha. Tunapozingatia nomino ambazo zinamilikiwa na kihusishi, basi tutaweza kudai kwamba Kiswahili ni lugha yenye vihusishi vya kabla ya nomino pekee. Hii ni kwa sababu hata kwenye virai nomino vyenye vihusishi vya a-unganifu, nomino inayotangulia kihusishi haitajumulishwa kama sehemu ya kirai kihusishi.

Hata hivyo, bado kuna kanuni ambazo zitakuwa na matatizo tunapozungumzia lugha ya Kiswahili kwa sababu Kiswahili kama lugha ambishi bainishi huwa na muundo changamano wa uambishaji.

HITIMISHO

Utafiti wetu umehusu ukiukaji wa kanuni bia za Greenberg katika miundo ya tungo zenye vihusishi katika lugha ya Kiswahili. Tumechambua kanuni bia zilizohusisha vihusishi huku tukizingatia sheria za utendakazi za Greenberg. Tumehitimisha kwa kauli kuwa, ijapokuwa lugha ya Kiswahili inatii baadhi ya vipengele vya kanuni bia za Greenberg kuhusu uwekaji wa vihusishi, kuna vipengele vingine ambavyo vya kanuni hizo ambazo havidhihiriki kutokana na kuwa Kiswahili kina vihusishi vya kabla na baada ya nomino.

MAREJELEO

- Abraham, W., Givón, T., & Thompson, S. A1 (1995). *Discourse, Grammar and Typology: Papers in honor of John WM Verhaar* (Vol. 27). Amsterdam. John Benjamins Publishing.
- Beliavsky, N. (2004). Review of “Metaphor, Culture and World View: The Case of American English and the Chinese Language” by Dilin Liu. *Journal of Asian Pacific Communication*, 14(2), 355–361.
- Bloomfield, A. L. (1933). *Language*. New York Holt: Rinehart & Winstorn
- Dryer, M. S. (1991). SVO languages and the OV: VO typology1. *Journal of linguistics*, 27(2), 443-482. (Published online) DOI: [10.1017/S0022226700012743](https://doi.org/10.1017/S0022226700012743).
- Greenberg, J. (1963). Some universals of grammar with particular reference to the order of meaningful elements. In J. Greenberg, (Ed). *Universals of Language*. 73-113. London: MIT Press.
- Greenberg, J. H. (1966). Synchronic and diachronic universals in phonology. *Language*, 42(2), 508-517.
- Hockett, C. F. (1961). Linguistic Elements and their Relations. *Language*, 37(1), 29-53.
- Hopper, P. J., & Traugott, E. C. (2003). *Grammaticalization*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Huddleston, R. (2000). *Introduction to the Grammar of English*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Huddleston, R., & Pullum, G. K. (2002). *The Cambridge grammar of the English language*. Cambridge, UK: CUP
- Katamba, F., & Stonham, J. (2006). *Morphology* (2nd Edition). New York: Palgrave Macmillan Publishers.
- Keenan, E. (1978). Negative Coreference: Generalizing Quantification for Natural Language. *Formal Semantics and Pragmatics for Natural Languages*, 77-105.
- Koopman, H. (2000). Prepositions, postpositions, circumpositions and particles: The structure of Dutch PPs. In H. Koopman (Ed.), *The Syntax of Specifiers And Heads*, 198-256. London: Routledge.
- Kuno, S. (1974). The position of relative clauses and conjunctions. *Linguistic Inquiry*, 5(1), 117-136.
- Lefebvre, C. & Brousseau, A. (2001). *A grammar of Longbe*. Berlin: Mouton de Gruyter.

Luraghi, S. (2003). *On the Meaning of Prepositions and Cases: The Expression of Semantic Roles in Ancient Greek*. Amsterdam/Philadelphia: John Benjamins Publishing Company.

O'Dowd, E. M. (1998). *Prepositions and Particles in English: A Discourse-functional Account*. New York: Oxford University Press.

Riemsdijk, V. H. (2020). *A Case Study in Syntactic Markedness: The Binding Nature of Prepositional Phrases* (Vol. 4). London: The Peter de Ridder Press.

Tyler, A., & Evans, V. (2003). *The Semantics of English Prepositions: Spatial Scenes, Embodied Meaning, and Cognition*. Cambridge: Cambridge University Press.